## Biashara ya Kaboni

Biashara ya Kaboni ni biashara inayoibuka duniani ambayo ni moja ya utaratibu wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Hata hivyo, kuna uelewa mdogo kuhusu biashara ya Kaboni kwa Watanzania wengi. Hali hii inasababisha kutopata fursa zinazoletwa na biashara hii. Kwa hiyo, andiko hili linajibu baadhi ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu Biashara ya Kaboni nchini.

***Mradi wa biashara ya Kaboni ni nini?***
Mradi wa Kaboni maana yake ni mradi wowote unaotekelezwa kwa ajili ya kuzalisha *Viwango vya Kaboni* (Carbon credits) vinavyotambulika kimataifa

***Viwango vya Kaboni ni nini?***
Viwango vya Kaboni (Carbon credits) maana yake ni kiasi cha tani moja ya hewa ya Kabonidayoksaidi au kiasi kinacholingana na hicho cha hewa nyingine ya gesijoto kinachopunguzwa kwa ajili ya kuuzwa kwenye Biashara ya Kaboni.

***Ni shughuli zipi zinafaa kuanzisha Biashara ya Kaboni?***
Sekta ambazo miradi ya Kaboni inaweza kuanzishwa ni pamoja na: nishati, uchukuzi, misitu na udhibiti wa taka, viwandani na matumizi ya bidhaa na kilimo.

***Sekta ya Nishati***
Maeneo yenye fursa ni pamoja na:

- Matumizi ya vyanzo vya nishati safi kwa ajili ya uzalishaji wa umeme kama vile joto ardhi, upepo, mawimbi, jua, gesi asilia, umeme maji na tungamotaka;
- Teknolojia nafuu na zenye ufanisi za nishati ya kupikia; na
- Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya nishati.

***Sekta ya Usafirishaji***
Maeneo yenye fursa ni pamoja na:

- Matumizi ya nishati safi katika vyombo vya usafirishaji;
- Mifumo ya Usafiri wa Umma wa Haraka;
- Usafiri usio wa vyombo vya moto; na
- Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya usafirishaji.

***Menejimenti ya Taka***
Maeneo yenye fursa ni pamoja na:

- Matumizi ya njia za kisasa za manejimenti ya taka ikiwa ni pamoja na kuimarishwa kwa matumizi ya uvunaji wa methani kutoka kwenye madampo;
- Uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia za kuzalisha nishati kutokana na taka;
- Uvunaji wa methani unaotokana na kutibu maji taka; na
- Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya usimamizi wa taka.

***Sekta ya Misitu***
Maeneo yenye fursa ni pamoja na:

- Kupunguza uzaishaji wa gesijoto kutokana na upotevu na uharibifu wa misitu;
- Kuimarisha usimamizi wa misitu;
- Uhifadhi wa misitu;
- Upandaji Miti au Upandaji Miti Upya;
- Urejeshaji wa mifumo ya ikolojia iliyoharibika;

- Fursa za kaboni ya bluu kama vile uhifadhi wa mikoko, nyasi za baharini, pamoja na shughuli nyingine za uchumi wa bluu zinazofyonza kaboni kutoka angani; na
- Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya misitu.

***Sekta ya shughuli za uzalishaji viwandani na matumizi ya bidhaa***
Maeneo yenye fursa ni pamoja na:
- Matumizi ya mbinu na teknolojia bora za uzalishaji viwandani;
- Vyanzo anuai vya nishati na matumizi ya nishati mbadala;
- Udhibiti wa taka za viwandani; na
- Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya shughuli za uzalishaji viwandani na matumizi ya bidhaa.

***Sekta ya Kilimo***
Maeneo yenye fursa ni pamoja na matumizi ya mbinu za Kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi kama vile:
- kuboreshwa kwa kilimo cha ukwatuaji,
- udhibiti wa mmomonyoko wa udongo,
- matumizi ya matandazo,
- matumizi ya mbolea vunde na biochar,
- usimamizi wa malisho,
- uvunaji wa maji, na
- kilimo cha uhifadhi, kilimo mseto, na uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya kilimo.

***Nani wananunua Viwango vya Kaboni?***
Ni mashirika, watu binafsi au serikali wanaotaka waonekane kuwa viwango vyao vya uzalishaji wa gesijoto wanavifanyia kazi ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi.

***Je bei ya Viwango vya Kaboni ikoje kwa sasa?***
Bei ya Viwango vya Kaboni hubadilika kutegemeana na nguvu ya Soko na aina ya mradi.

***Nifanye nini ili nijiunge na Biashara ya Kaboni?***
Mchakato wa kuanzishwa kwa biashara ya Kaboni umeainishwa kwenye Kanuni na Mwongozo wa Biashara ya Kaboni uliotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 2022 na marekebisho yake. Nyaraka hizi zinapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais https://www.vpo.go.tz/ au tovuti ya Kituo cha Kitaifa cha Kuratibu Kaboni https://www.ncmc.sua.ac.tz/tanzania-carbon-trading-regulations.

***Nani wa kuwasiliana naye unapohitaji msaada?***

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Makamu wa Rais,
Eneo la Mtumba,
S.L.P. 2502, Barua pepe: ps@vpo.go.tz, Simu: (255) (22) 2163400-19 au (255) (75) 6140140
**40406 DODOMA.**

Mkurugenzi,
Kituo cha Kitaifa cha Kuratibu Kaboni,
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
S.L.P 3000, Barua pepe: ncmctanzania@sua.ac.tz, Phone 255 23 2603511-4.
**MOROGORO.**